SHULE YA UPILI YA_____
JINA……
NAMBARI YAKO……KIDATO……..
MKONDO……..TAREHE……..

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA

KISWAHIILI
102/2 NA FASIHI SIMULIZI
FEBRUARI/MACHI 2021
MUDA: SAA 2 ½

MTIHANI WA DIRA 27

KIDATO CHA KWANZA

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA

MAAGIZO

(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(c) Jibu maswali yote.
(d) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
(e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
(f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
(g) Karatasi hii ina kurasa NNE zilizopigwa chapa.
(h) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	**UPEO**	**SEHEMU**	**ALAMA**
1	15	UFAHAMU	
2	40	LUGHA	
3	10	ISIMUJAMII	
4	15	FASIHI SIMULIZI	
JUMLA	**80**		

1. UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Tangu zama kongwe za mawe maisha ya binadamu yamepitia katika awamu mbalimbali za kimaendeleo; yawe ya kisayansi, kiuchumi, kijamii au hata kisiasa. Katika kipindi chote ambacho binadamu ameishi katika ulimwengu huu, utamaduni umekuwa sehemu muhimu ya maisha yake. Utamaduni huu unaweza kuangaliwa kwa namna mbalimbali. Upo utamaduni finyu ambao unahusisha jamii moja dogo mathalan, kabila, ukoo au eneo dogo. Kwa upande mwingine kuna utamaduni pana ambao unaihusisha jamii nzima. Mathalan, nchi fulani inaweza kuwa na matendo, imani, thamani na fikira ambazo ni msingi mkubwa katika nchi hiyo. Hizi huwa msingi wa utamaduni wa kitaifa. Utamaduni huu ndio ambao unamtenga raia wa nchi moja na raia wa nchi nyingine. Utamaduni wa kitaifa ni nguzo muhimu ya uzalendo wa wanataifa maalum; unawatambulisha na wanauonea fahari. Vipengele vya utamaduni wa kitaifa huweza kutokeza kwa njia mbalimbali kama mavazi, vyakula, lugha, itikadi au hata mtazamo wa raia wa nchi mahsusi. Tumbi kubwa ya nchi za ulimwengu huwa na utamaduni unaozitambulisha na ambao humfanya raia ajinabi kuweza kuwatambua raia hao. Utamaduni ni kitovu cha uhai wa jamii yoyote ile. Licha ya ukweli huu, ni muhimu, inahalisi kutambua kuwa maisha ya binadamu huathiriwa na kani mbalimbali zinazotokea katika mazingira yake ya kila siku. Kani hizi huweza kuwa vyanzo vya mabadiliko ya sifa fulani zinazohusishwa na utamaduni wake. Maendeleo ya kiwakati ambayo huenda sambamba na mahitaji anuwai ya kimaisha huweza kuwa chanzo cha kuachwa kwa tamaduni fulani. Hata hivyo, binadamu sio sifongo ambalo hufyonza maji yote, maji machafu na maji safi pasi na kubagua. Binadamu mwenye akili razini anapaswa kuchuja na kutathmini ni amali au thamani zipi mpya ambazo anaweza kuzichukua na labda kupuuza baadhi ya thamani za kale zisizomfaa. Kigezo kikuu kinachomsaidia ni kutambua mahitaji yake sambamba na wakati anamoishi. Mathalan, katika maisha ya zamani, uchumaji ulitegemea ubabe kwa kiasi kikubwa lakini siku hizi ubabe sio kigezo cha uchumaji kwa kiasi kikubwa. Akili ni msingi mkubwa sana siku hizi katika uchumaji au kutarazaki. Inahalisi basi kupuuza sifa za kitamaduni ambazo zinaelekea kuutilia mkazo mkubwa kwenye matumizi ya nguvu au ubabe. Yapo matendo mengi katika jamii ambayo yalidhibitiwa na imani za kishirikina kabla ya nuru ya elimu kulimulika giza la ujinga lilitotamalaki katika jamii. Ikiwa jamii itaendelea kuyatenda matendo hayo basi ile itakuwa ni jamii ambayo, kama pia, imezunguka palepale. Ile itakuwa ni jamii ambayo imeshindwa kuendelea.

MASWALI

a) Taarifa hii inahusisha utamaduni na wakati kwa jinsi gani? (Alama 2)

b) Eleza uwili unaojitokeza katika utamaduni (alama 2)

c) Eleza dhima ya utamaduni ukirejelea taarifa (Alama 3)

d) Taja methali moja ukieleza matumizi yake inayofumbata ujumbe ulioko katika taarifa hii (Alama 2)

e) Eleza mambo yanayopewa kipau mbele katika mchujo wa utamaduni (alama 2)

f) Uchumaji katika jamii umeathiriwa na wakati. Tathmini (alama 2)

g) **Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kama vilivyotumika katika taarifa husika.**(alama 2)

(i) Raia ajinabi

(ii) Giza la ujinga lililotamalaki

2. MATUMIZI YA LUGHA

a) Majina haya hupatikana katika ngeli gani (alama 4)

(i) Sukari .....

(ii) Kiongozi .....

(iii) Gari.....

(iv) Kalamu .....

b) **Andika sentensi moja yenye viungo vifuatavyo** (alama 3)

(i) Kikanushi
(ii) Kiima katika nafsi ya pili wingi
(iii) Mtendewa katika nafsi ya tatu umoja
(iv) Wakati uliopita
(v) Kauli ya kutendea
(vi) Shina / Mzizi wa kitenzi

c) **Tunga sentensi ukitumia neno 'haya' kama** (alama 3) ***BND***

(i) Kiwakilishi

(ii) Nomino

(iii) Kivumishi

d) Tambua vielezi katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Mwanafunzi mzuri ni yule afanyaye mazoezi vizuri kila siku shuleni

e) **Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi**

Wakili alimtahadharisha mshukiwa kwamba asingemwarifu ukweli wote kuhusu kesi hiyo asingemwakilisha

(alama 2)

f) **Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa na udogo**

Mbuzi yuyu huyu alikula mimea ya mwanamke yule (alama 2)

g) **Tumia 'o' rejeshi ya mazoea katika sentensi ifuatayo.**

Mti ambao ulikatwa ulipelekwa kiwandani (alama 1)

h) **Onyesha kundi nomino na kundi tenzi katika sentensi ifuatayo**

Mwanafunzi wetu mwerevu alitembea haraka lakini hakufika mapema (alama 2)

i) **Onyesha nomino katika sentensi ifuatayo .**
Kucheza kwa Juma kulikipa furaha kikosi cha askari (alama 4)

j) **Geuza kitenzi kiwe jina ukikanusha**
Juma ameoa mwanamke mrembo mithili ya hurulaini (alama 1)

k) **Tunga sentensi moja ukionyesha neno lililo na silabi moja** (alama 1)

l) **Eleza jinsi neno 'kwetu' lilivyotumika katika sentensi zifuatazo** (alama 3)
(i) Juma ameenda <u>kwetu.</u>

(iii) <u>Kwetu</u> ni kule

(iv) Mahali <u>kwetu</u> ni kule

m) **Tunga sentensi mbili ukionyesha kiimbo igizi na arifu.** (alama 2)

n) **Eleza maana na matumizi ya methali ifuatayo**
Angaruka juu kipungu hafikilii mbinguni (alama 2)

o) **Andika visawe mwafaka** (alama 2)
(i) Hau……
(ii) Bohari…..**.....**

p) **Tunga sentensi ukitumia semi zifuatazo** (alama 2)
(i) Piga bweu**.....**
(ii)Kazi ya papara papara……

q) **Tumia neno hili kutunga sentensi tatu zenye maana tofauti**
Kina (alama 3)

3. ISIMU JAMII
a) Eleza maana ya Isimu jamii (alama 1)

b) **Eleza maana ya dhana zifuatazo za simu ya jamii** (alama 6)
(i) Msimbo

(ii) Lafudhi.

(iii) Lahaja.

c) Fafanua sifa nne za lugha ya darasani

4. FASIHI SIMULIZI

a. Fasihi simulizi na fasihi andishi huoana. Thibitisha kwa hoja tano. Alama 10

b. Tambua sifa tano za mwimbaji mzuri. Alama 5